# MAAJABU YA KUSOMA VITABU

**GODIUS RWEYONGEZA**

**(songambele)**

Jinsi kusoma vitabu kunavyoweza kukutengenezea utajiri wa kifedha, kiakili, kiafya, kimwili na kiroho

VITABU VINGINE VYA MWANDISHI HUYU

1. KUTOKA SIFURI MPAKA KILELENI

2. TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA (toleo la kwanza)

3. NYUMA YA USHINDI;kuna kushindwa, kushindwa, kkushindwa.

4. MAMBO 55 YA KUZINGATIA KABLA YA KUANZISHA BIASHARA

5. JINSI YA KUIBUA UBUNIFU ULIO NDANI YAKO

6. BARUA YA WAZI KWA WAZAZI NA WALEZI WA WATOTO

7. TATIZO SI RASILIMALI ZILIZOPOTEA (toleo la 2

8. TIMIZA NDOTO ZAKO

9. MAKOSA 10 WANAYOFANYA WAKULIMA, NA JINSI YA KUYAEPUKA

**Maajabu Ya Kusoma Vitabu**
©GODIUS RWEYOGEZA

Toleo la kwanza (nakala laini) Septemba 2019
MOROGORO, TANZANIA

Toleo la pili (nakala ngumu) Juni 2020
DAR ES SALAAM, TANZANIA

Haki zote zimehifadhiwa
Hakuna sehemu yoyote ile ya kitabu inaruhusiwa kutolewa upya, kunakiliwa au kuhamishwa kwa namna yoyote ile. Iwe ni kwa njia zinazofahamika sasa hivi au zitakazogunduliwa hapo baadaye bila idhini ya mwandishi.

:

**Mawasiliano**:

Simu: 0755848391

Barua pepe:songambele.smb@gmail.com

Tovuti: www.songambeleblog.blogspot.com

# Mitandao ya kijamii

JIUNGE NAMI KWENYE MITANDAO YA KIJAMII

YOUTUBE: BONYEZA HAPA

FACEBOOK: BONYEZA HAPA

INSTAGRAM: BONYEZA HAPA

TWITTER: BONYEZA HAPA

# TUNUKU

Maalumu kwa wale wote ambao ni wapenzi wa kusoma vitabu.

Maalumu pia kwa wale ambao wangependa kusoma vitabu ila hawajui namna ya kusoma na wanakosa nidhamu na muda wa kusoma vitabu.

Kwa wazazi wangu, ambao siku zote wamekuwa mstari wa mbele na wamekuwa wakinitia moyo wa kusoma. Hata siku moja hawajawahi kusema chochote cha kunikatisha tamaa kutokana na tabia yangu ya kupenda kusoma iliyopitiliza.

# NUKUU MUHIMU

Mjinga wa karne ya 21 sio yule ambaye hajui kusoma na kuandika. Mjinga wa karne hii ni yule ambaye anajua kusoma na kuandika ila hasomi wala kujifunza- Godius Rweyongeza

Wale ambao hawasomi, ni sawa na wale ambao hawajui kusoma kabisa- Methali ya kichina

Siku zote kuwa unasoma, kitabu ni lenzi za kuiona dunia vizuri.

Watu wanashangaza sana, wanajali sana kuhusu utapiamlo wa mwili kwa kuhakikisha kuwa wanapata mlo kamili. Ila hawajali kuhusu utapiamlo wa akili ambao unatokana na kutosoma vitabu. Na utapiamlo wa akili una athari kubwa zaidi kuliko hata utapiamlo wa mwili.

Viongozi ni wasomaji ( leaders are readers)

Chumba ambacho hakina vitabu ni sawa na mwili ambao hauna roho

Rafiki yangu wa kweli ni mtu ambaye atanipa kitabu- Abharam Lincoln

Siku zote soma vitabu ambavyo watu watasema kweli huyu alikuwa msomaji mzuri wa vitabu, ikitokea ukaaga dunia ukiwa katikati ya kusoma kitabu-P.J.O'Rourke

Kitu pekee ambacho unapaswa kujua kwa uhakika ni mahali ilipo maktaba-Albert Einstein

Aliyesema kwamba, ukitaka kumficha mwafrika kitu, unapaswa kukiandika katika kitabu, alikuwa msomaji mzuri wa vitabu –Godius Rweyongeza

yaliyomo

Maajabu Ya Kusoma Vitabu ........................................3

Mitandao ya kijamii ........................................4

TUNUKU ........................................5

NUKUU MUHIMU ........................................6

UTANGULIZI ........................................10

SASA KWA NINI WATU HAWAPENDI KUSOMA VITABU........................................15

KWA NINI UNAPASWA KUSOMA VITABU ........................................24

WAPI NITAPATA MUDA WA KUTOSHA KUSOMA VITABU?........................................32

IDADI YA VITABU UNAVYOPASWA KUWA UMESOMA ........................................39

HIVI NDIVYO UNAWEZA KUSOMA KITABU KIMOJA TU KILA MWEZI ........................................40

JINSI YA KUONGEZA SPIDI YA USOMAJI........................................41

WANASEMAJE WATU WENYE BUSARA NA WALIOFANIKIWA KUHUSU KUSOMA VITABU?........................................45

WAULIZE WANASOMA NINI ........................................47

KAMA HUSOMI HUTAKUJA KUSOMWA........................................48

NAMNA YA KUFANYA USOMAJI UWE SEHEMU YA PILI YA MAISHA YAKO........................................49

NI KWELI VITABU VINASAIDIA?........................................51

MAKTABA ZA KARNE YA 21 ........................................53

NAKALA NGUMU NA NAKALA TETE...........................55

VITABU VILIVYOSOMWA ...........................................56

WATU WAKIWASHA RUNINGA WEWE JIFUNGIE USOME KITABU .....................................................57

JINSI UNAVYOWEZA KUJENGA TABIA YA KUSOMA KWENYE MAZINGIRA YENYE RUNINGA. ...................60

JINSI YA KUWAJENGEA WATOTO WAKO TABIA YA KUSOMA VITABU ..................................................61

KITU MUHIMU KATIKA USOMAJI WA VITABU .........62

TUBADILI ZAWADI TUNAZOTOA ...............................64

TUBADILI PIA VIKUNDI PIA VYA KUPIGA SOGA......................66

AKILI NENE vs MWILI MNENE .....................................67

UNAENDA KUANZA KUSOMA VITABU GANI?...........69

KITU HIKI HUWEZI KUJIFUNZA KWENYE KUSOMA VITABU ...73

HITIMISIHO: MAMBO NA VIJIMAMBO .........................75

KUHUSU MWANDISHI ......................................................76

KUHUSU KITABU:............................................................77

# UTANGULIZI

Siku chache baada ya kuwa nimejiunga na chuo kila nilipokutana na mtu, nilihakikisha namwambia kuhusu umuhimu wa vitabu na kwa nini kila mtu anapaswa kusoma vitabu. Kipindi hicho ndio nilikuwa ninaendelea kusoma kitabu cha *Think And Grow Rich* huku nikiwa nimemaliza vingine vingi miongoni vikiwa ni vitabu vya *Rich Dad Poor Dad* na *Cashflow Quadrant*. Katika maongezi yangu sikusahau kutoa nukuu za akina Albert Einstein, Donald Trump, Robert Kiyosaki, Napoleon Hill na wengine wengi. Kila niliyeongea naye kuhusu usomaji wa vitabu, alionekana amependa na ataanza kusoma vitabu kuanzia siku hiyo.

Nakumbuka kuna watu nilikaa na kuwapa umuhimu wa kusoma vitabu na namna utakavyobadili maisha yao baadaye nikawauzia kitabu cha *Biashara Ndani Ya Ajira* ila hawakuwahi kukisoma. Kila aliyeshawishika kusoma vitabu nilikuwa namtumia vitabu vitatu ambavyo ni *Think And Grow Rich, Rich Dad Poor Dad* pamoja na *The Richest Man In Babylon*. Lakini tatizo lilibaki kwamba watu hawa walikuwa hawasomi hivi vitabu.

Kadiri muda ulivyoenda niligundua kwamba nilitumia muda mwingi sana kuwashawishi watu kusoma vitabu na kuwatumia vitabu ila walikuwa hawasomi. Nikaanza kujiuliza nifanyeje? Baada ya kuona juhudi zangu

hazizai matunda ya maana nikaacha kutumia nguvu kubwa kuwashawishi watu kusoma vitabu.

Nikaamua kwamba kwa sababu mimi napenda mabadiliko basi nitakuwa mabadiliko ambayo nataka niyaone kwenye jamii na nitaonesha mfano kwenye kusoma vitabu na kufanya kwa vitendo yale niliyojifunza kenye vitabu ili nipate matokeo ya tofauti ambayo wengine hawapati. Na watu wakiniuliza nimewezaje, basi nitatumia nafasi hiyo kuwashawishi kusoma vitabu.

Ila niseme tu kwamba kila mara nilipopata nafasi ya kuwaambia watu kuhusu usomaji wa vitabu, basi sikuacha kufanya hivyo na nilikuwa nikiwasisitiza ni vitabu gani wanaweza kusoma. Nimepata wasaa huo tena kupitia kitabu hiki, ninaenda kukwambia kwa undani kuhusu usomaji wa vitabu na kwa nini unapaswa kuanza kusoma sasa hivi. Tofauti yako wewe na hao wengine ni kwamba kwenye kurasa za kitabu hiki hapa ninaenda kukupa dozi nzima juu ya usomaji wa vitabu. Ukiifanyia kazi dozi hii nina uhakika maisha yako yatabadilika na kuwa ya kipekee sana.

Baada ya muhula wa kwanza wa chuo kuisha, nakumbuka nilitengenza kundi la wasapu na kuliita AFRICA BOOKWORMS CLUB (ABC), kwa ajili ya watu waliokuwa wanapenda kusoma vitabu tu. Na

kwenye hili kundi nililenga waingie wanachuo wengi kadiri iwezekanavyo, maana, niliamini wanachuo wakibadilika, basi jamii nzima itapata urahisi wa kubadilika. Na kweli waliingia wengi. Ndani ya masaa yasiyopungua matatu kundi lilikuwa na watu wasiopungua 130, ambao walikuwa wanasubiri wapewe utaratibu wa kusoma vitabu kwenye kundi hilo jipya. Niliweka lengo kubwa sana ambalo lilikuwa gumu kwa wengi. Lengo lilikuwa ni kusoma vitabu viwili kwa wiki. Na vitabu ningetuma mimi kwenye kundi ambapo kila mtu angesoma na kutuma kitu alichojifunza kwenye kitabu kila siku.

Kila siku asubuhi nilikuwa natuma makala ya kuhamasisha watu kuhusu kusoma na kuwataka wasome kitabu kilichotumwa kwenye kundi. Baadhi ya makala nilizotuma kwenye kundi hilo kwa wakati huo, utakutana nazo kwenye kitabu hiki ila zamu hii zimeboreshwa na kuongezwa nyama zaidi. Kitabu cha kwanza nilichotuma kwenye kundi kilikuwa ni kitabu cha *Be Obssessed Or Be Average,* mwandishi wake ni Grant Cardone. Kilichonishangaza ni kuwa watu waliojiunga kwa hiari wakijua kwamba watakuwa wanasoma vitabu hawakutaka kusoma. Mwanzoni wachache walisoma ila mwishoni nikabaki mimi na rafiki yangu Edius Katamugora. Baada ya kuona pia natumia nguvu kubwa

sana huku niliamua kuachana na kitu hiki na kuliacha kundi. Watu waliondoka taratibu na baadaye nikwaondoa wengine waliobaki. Nikiangalia safari yote hii ya kutaka kuwashirikisha maarifa ya kusoma basi naona kuna kosa ambalo nilifanya ambalo laiti nigelifanyia kazi kundi hilo lingekuwepo mpaka leo hii. Pengine na wewe leo hii ungenitumia ujumbe ukinitaka nikuunge kwenye kundi hilo ili tuungane kusoma vitabu kama jumuiya ya watu wanaofikiri nje ya boksi. Ningewaondoa wale waliokuwa hawasomi na kubaki na wale wachache waliokuwa wanasoma na baadaye wale wachache wangesambaza ujumbe kwa marafiki zao wasomaji. Tukatengeza jumuiya ya wasomaji wa vitabu Afrika. Maana siku zote vitu vya aina moja huwa vinapenda kuwa pamoja. Hili ni kosa ambalo nilifanya kipindi hicho.

Lakini niseme tu kwamba lengo langu la kutaka kuwafikia wasomaji zaidi bado halijaisha. Maana kila mara ambapo nimekuwa nakutana na mtu na kitabu basi huyo nimekuwa nikipata nafasi ya kuongea naye na kutaka kujua zaidi kutoka kwake. Imani yangu na wewe utakuwa msomaji mzuri sana. Pengine wewe ndiwe unakuja kuwa mwanachama mpya wa AFRICA BOOKWORMS CLUB (ABC).

Karibu sasa uingie ndani kwenye kurasa za kitabu hiki ili upate kujifunza zaidi kuhusu kusoma vitabu. Fanyia kazi utakachojifunza ili uweze kupata matokeo maana kama ambavyo Albert Einstein anasema; hauwezi kupata matokeo ya tofauti kama utaendelea na fikra zile zile zilizokufanya upate matokeo ya sasa hivi. Njia ya kipekee sana kwenye kubadili fikra zako basi ni kusoma vitabu. Vitabu vina uwezo wa kubadili kilaza kuwa gwiji, vina uwezo wa kubadili mtumwa kuwa kiongozi. Vitabu vitabadili namna unavyoongea, tembea, kutenda na kuishi maisha yako kiujumla. Nakubaliana na Charlie "Tremendous" Jones aliyesema miaka mitano ijayo utakuwa jinsi ulivyo isipokuwa kwa vitu viwili tu, vitabu unavyosoma na watu ambao unakutana nao. Je, upo tayari?

KUPATA MAFUNZO ZAIDI KUHUSU USOMAJI WA VITABU BONYEZA HAPA NA USUBSCRIBE KWENYE YOU TUBE CHANNEL YANGU

# SASA KWA NINI WATU HAWAPENDI KUSOMA VITABU

Ukiingia kwenye daladala, basi, au usafiri mwingine wowote, utagundua kwamba asilimia kubwa ya watu kwenye eneo hilo wameshika simu, na kila mtu yuko bize anachati au anaangalia picha mtandaoni. Sasa unakaa na kujiuliza kwa nini watanzania hawapendi kusoma vitabu? Kwa nini muda huu ambao mtu anafanya vitu ambavyo havina manufaa asiutumie kusoma kitabu ambacho kina manufaa makubwa kwake. Kwa nini watu wanakimbilia kupiga selfie ili waweke kwenye mitandao ya kijamii zaidi ya wanavyokimbilia kusoma vitabu? Sasa hapa kuna baadhi ya sababu zinazowafanya watu wasisome.

**1. Watu wameaninishwa kwamba ukitaka kumficha mwafrika kitu basi kiandike kwenye kitabu**. Na hili nimekuwa nikiligundua baada ya kuwa nimewashauri watu juu ya usomaji wa vitabu na umuhimu wake ila mwisho unasikia mtu anakwambia kwamba ila kwa sisi watanzania kusoma vitabu ni kitu kigumu sana.

Ninachoamini aliyesema;“*Ukitaka kumficha mwafrika kitu basi kiandike kwenye kitabu”* alikuwa ni msomaji

mzuri wa vitabu na hivyo aliona ni kwa jinsi gani waafrika walikuwa wametumbukia kwenye matatizo ambayo wangekuwa wameyapatia suluhisho kwa kusoma vitabu. Hivyo, akaamua kusema "**ukitaka kumficha kitu mwafrika basi kiandike kwenye kitabu**".

Je, wewe unakubaliana na hili? Naamini kama bado unasoma hapa sio mtu wa kukubaliana na usemi huu ambao wengi wameaminishwa. Jiweke miongoni mwa watu ambao kitu kikifichwa kwenye kitabu lazima tu wakigundue.  Labda, mtu atafute mbinu nyingine ya kukuficha kitu lakini sio kwenye kitabu. Na kwa sababu vitabu ni miwani ya kuona kusikoonekana basi niseme tu hakuna namna mtu ataweza kukuficha kitu.

2. Kuna wengine wanaamini kwamba **hawana muda** wa kusoma vitabu na hivyo hawasomi na hawatakaa wasome vitabu. Nimewahi kumpa mzee wa makamo (karibu afikishe miaka 50) kitabu ambacho

KUPATA VITABU VYANGU VINGINE BONYEZA HAPA

https://www.getvalue.co/home/seller_collection/393

JIUNGE NAMI KWENYE MITANDAO YA KIJAMII

YOUTUBE: BONYEZA HAPA

FACEBOOK: BONYEZA HAPA

INSTAGRAM: BONYEZA HAPA

TWITTER: BONYEZA HAPA

## HITIMISIHO: MAMBO NA VIJIMAMBO

Mpaka hapa tumeshajifunza mambo mengi kuhusu usomaji wa vitabu. Hapa kwenye hitimisho ninaenda kukupa hadithi fupi fupi kuhusu usomaji wa vitabu ambazo nimekuwa nikikutana nazo. Nyingine inawezekana tayari umezisikia. Nyingine nimezisikia au zimenitokea mimi tu.

### Kusoma sana kunakufanya uwe kichaa

Hii ni hadithi ambayo nimeisikia sana nikiwa mtoto. Wanasema kwamba ukisoma sana ndio hivyo unaweza kuwa kichaa.

Binafsi mpaka leo hii sijaona mtu wa namna hii. Na wala sijaona utafiti wa kisayansi ambao unasema kwamba kusoma sana kunakufanya uwe kichaa. Labda kama

wewe una ushahidi unaweza kunitumia kupitia 0755848391 (wasapu tu)

**Kusoma na kipara**

Kuna kijihadithi kingine ambacho kinasema kwamba ukisoma sana unakuwa na kipara. Labda wewe pia utakuwa umeona kitu kama hicho ili uniambie.

**KUHUSU MWANDISHI**: Godius Rweyongeza (Songambele) ni mhamasishaji, mwandishi na mjasiliamali ambaye amejikita kuhakikisha kuwa anawasaidia watanzania wengi kuwa na maisha bora kupitia kazi zake. Na amekuwa akifanya hivi kupitia maandishi yake, semina na mafunzo kwa watu na taasisi mbalimbali.

Mtandao wake wa SONGA MBELE BLOG (www.songambeleblog.blogspot.com), umeweza kuwasaidia wengi kubadili maisha yao na kuchukua hatua za kipekee maishani mwao.

Aidha, vitabu vyake ambavyo vipo 10 mpaka unapopokea kitabu hiki hapa, vimesaidia maelfu kwa maelfu kubadili fikra zao, kupangilia maisha yao na kuchukua hatua za kitofauti. Wengine wameanzisha biashara na wengine kukuza biashara zao baada ya

kusoma maandishi ya Godius Rweyongeza (Songambele). Waliokuwa wamekata tamaa, wamepata tumaini jipya la maisha na kupangilia upya maisha yao upya.

Zamu hii Songambele amekuja kwako kupitia kitabu hiki hapa cha MAAJABU YA KUSOMA VITABU.

**KUHUSU KITABU:** Ukitaka kumficha mwafrika kitu basi kiandike katika kitabu. Huu ni usemi ambao umekuwa maarufu miongoni mwa watu kiasi kwamba umekuwa sehemu ya pili ya maisha yao. Na asilima kubwa ya watu ambao nimekuwa nikiongea nao wanathibitisha kuukubali usemi huu. Ndio maana utasikia watu wakisema, SISI watanzania au waafrika huwa hatusomi vitabu. Na mtu anatumia neno SISI kama vile ni jamii yote kabisa ambayo haisomi vitabu.

Kwenye kurasa za kitabu hiki hapa cha MAAJABU YA KUSOMA VITABU unaenda kujifunza jinsi kusoma vitabu kunavyoweza kubadili maisha yako. Kama umekuwa unapata shida ya kupata muda au hujui umuhimu wa kusoma vitabu, basi kitabu hiki hapa kimeeleza kiundani. Utajifunza namna ya kusoma vitabu vingi kwa muda mfupi, utajifunza pia mbinu za kukuwezesha kupata vitabu vizuri vya kusoma.

Sambamba na hayo, utakutana na watu ambao wamekuwa wakisoma vitabu na jinsi kusoma vitabu, kulivyobadili maisha yao. Ni wakati wako sasa kuhakikisha kuwa unajua umuhimu wa kusoma vitabu. Kitabu hiki hapa ni maalumu kwa wasomaji wa vitabu na wale ambao wangependa kusoma vitabu. Wazazi ambao wangependa kuwajengea watoto wao tabia za kusoma vitabu, basi ni wazi kuwa hamhitaji kutumia nguvu kubwa sana. soma kitabu hiki hapa na tumia mbinu zilizo kwenye kitabu hiki hapa. Basi.

Kwa wale wasomi ambao huwa mnasema kwamba mnajua kila kitu. Yaani, kuwa huwezi kusoma kitu chochote baada ya kuhitimu, hata gazeti. Naona hiki kitabu sasa kimekuja mkononi mwenu ili kuwapa mwangaza wa kuendelea kujifunza na kusoma zaidi. Kama ambavyo utagundua ndani ya kurasa za kitabu hiki ni kuwa, shuleni unafundishwa kusoma na kuandika, ila katika maisha, unapaswa kusoma, na kama husomi vitabu, basi wewe hauna tofauti yoyote na yule ambaye hajui kusoma wala kuandika.

Kwako wewe ambaye ungependa kusoma vitabu vingi kwa muda mchache, iwe ni kwa ajili ya kusoma maandiko mengi ya kiutafiti au kusoma tu kwa ajili ya kujifunza. kurasa za kitabu hiki hapa zimeeleza kiundani hayo yote.

**Mjinga wa karne ya 21 sio yule ambaye hajui kusoma na kuandika. Mjinga wa karne hii ni yule ambaye anajua kusoma na kuandika ila hasomi wala kujifunza-** Godius Rweyongeza

Watu wanashangaza sana, wanajali sana kuhusu utapiamlo wa mwili kwa kuhakikisha kuwa wanapata mlo kamili. Ila hawajali kuhusu utapiamlo wa akili ambao unatokana na kutosoma vitabu. Na utapiamlo wa akili una athari kubwa zaidi kuliko hata utapiamlo wa mwili

Siku zote kuwa unasoma, kitabu ni lenzi za kuiona dunia vizuri.

JIUNGE NAMI KWENYE MITANDAO YA KIJAMII

YOUTUBE: BONYEZA HAPA

FACEBOOK: BONYEZA HAPA

INSTAGRAM: BONYEZA HAPA

TWITTER: BONYEZA HAPA

HAKIKISHA UMEJIUNGA NAMI YOUTUBE KWA : BONYEZA HAPA